**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

# SCHOOL BASED ASSESSMENT

## KISWAHILI SEHEMU B na C

## Gredi ya 8

**SEPTEMBA 2024**

**Karatasi hii ina kurasa 11 zilizopigwa chapa.**

© KNEC 2024

**JINA LA MWANAFUNZI**_______________________________________________

**GREDI** ________________________________________________________________

**TAREHE**_______________________________________________________________

**MUDA: SAA 2**

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

**JEDWALI LA ALAMA**

**SEHEMU B**

| **SWALI** | **ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA** | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **SWALI** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** | **6** | **7** | **8** | **9** | **10** | **11** | **12** |
| **UPEO** | **1** | **1** | **1** | **1** | **1** | **1** | **1** | **1** | **1** | **1** | **1** | **1** |
| **ALAMA** | | | | | | | | | | | | |

**ZOEZI 4: SARUFI**

| **SWALI** | **13** | **14** | **15** | **16** | **17** | **18** | **19** | **20** | **21** | **22** | **23** | **24** | **25** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **UPEO** | **1** | **1** | **1** | **1** | **1** | **2** | **2** | **2** | **2** | **1** | **2** | **2** | **2** |
| **ALAMA** | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | |

| | **ZOEZI 5: KUANDIKA** |
|---|---|
| **SWALI** | **26** |
| **UPEO** | **4 -** Kiwango cha juu cha kutathminia<br>(Performance Level) |
| **ALAMA** | |

**SEHEMU C: FASIHI**

| | **ZOEZI 6: FASIHI SIMULIZI** | **ZOEZI 7: TAMTHILIA** |
|---|---|---|
| **SWALI** | **27** | **28** |
| **UPEO** | **10** | **10** |
| **ALAMA** | | |

**ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la* ***1*** *hadi la* ***4****.*

Linda aliwasili katika soko la Beibora mwendo wa saa kumi na mbili asubuhi. Ilikuwa kawaida kama sheria kwa Linda kufika sokoni humo kila Jumamosi. Hii ndiyo siku ambapo alikuwa akinunua bidhaa za kutumia kwa wiki nzima. Aliliwajibikia jukumu hilo ambalo lilikuwa lake. Mume wake, Bwana Teku, pamoja na watoto wao walibaki nyumbani wakishughulikia usafi.

Punde tu baada ya kuwasili sokoni, Linda alienda moja kwa moja hadi sehemu kulikouzwa matunda anuwai. Alinunua mapera, maparachichi na matikitimaji. Hata hivyo, hakubahatika kupata maembe ambayo ndiyo matunda waliyoyapenda zaidi. Alifahamishwa na muuzaji kuwa huo haukuwa msimu wa maembe, **akaridhia.** Linda aliendelea kununua bidhaa nyingine kwa kuongozwa na orodha aliyokuwa ameiandaa. Kila aliponunua bidhaa zozote, alitia alama ya mkwaju kwenye orodha hiyo.

Linda alitazama orodha yake akatambua hakuwa amenunua vyakula vya wanga. Katika pochi lake alikuwa amesalia na shilingi mia tano. Alifululiza hadi kulikouzwa viazi vitamu, mahindi, mihogo na ndizi. Kule, wauzaji walijitahidi kuwarai wateja kwa njia mbalimbali kununua bidhaa zao.
"Mihogo *freshi* kutoka shambani, bei ya asubuhi, karibu mama." Mwuuzaji mmoja alimuita Linda. "Mama, hivi hapa viazi vitamu. Vina virutubishi muhimu. Nitakuuzia kwa bei nafuu." Muuzaji mwingine alimuita. Linda alisikiliza kwa makini kile wauzaji hao walikuwa wakisema. Kadhalika, alikadiria ubora na bei ya bidhaa hizo. Alikata kauli akanunua viazi vitamu na ndizi kisha akashika njia kuelekea nyumbani.

1. Linda alikuwa na mazoea ya kufanya nini siku ya Jumamosi?
   ____________________________________________________________

2. Mnununzi ana jukumu la kununua bidhaa kulingana na hela alizonazo. Eleza jukumu lingine la mnunuzi kulingana na kifungu________________________

3. Unadhani ni nini kingetokea iwapo Linda angeenda sokoni bila orodha ya bidhaa?
   ____________________________________________________________

4. Neno **akaridhia** limetumiwa kwenye kifungu kumaanisha
   ____________________________________________________________

**Geuza ukurasa**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la **5** hadi la **8**.*

Zamani, Panya na Binadamu walikuwa marafiki wa chanda na pete. Waliishi pamoja katika nyumba moja iliyokuwa mkabala na msitu mkubwa. Waliishi kwa amani na kusaidiana kwa kila njia. Walifahamu fika kuwa udugu ni kufaana. Panya alikuwa askari kwa Binadamu. Alimkinga dhidi ya adui wa kila namna, si wadudu, si wanyama watambaao, si wezi...

Panya angeweza kuhisi miondoko ya wanyama kama vile fisi kutoka mbali kule-e-e. Angetoa sauti fulani iliyomwarifu Binadamu kuhusu hatari. Hapo, Binadamu angejihami mara moja kukabiliana na nduli huyo. Si hayo tu, Panya aliwala wadudu ambao walivamia nafaka ghalani. Binadamu naye alimlisha Panya makombo na kumpa malazi kwenye ghala lililojaa nafaka. Hali iliendelea hivyo hata wakati mmoja Panya akautia uhusiano wake na Binadamu kwenye mizani.

**"Kwa nini nile ukoko na chungu kimejaa chakula ndi?** Hivi kiumbe huyu haoni jinsi ninavyomsaidia?" Panya alijisemea.

Baada ya siku nyingi za kuwaza na kuwazua, Panya alianza kuumauma magunia ya nafaka na kujisaidia kwa chochote kilichokuwamo. Mwanzoni, Binadamu alidhani kuchanika kwa magunia kulitokana na ukuukuu wayo. Lakini hali ghalani ilizidi kuwa mbaya.

Jioni moja, Binadamu alijitia uchovu baada ya chajio, akaomba kupumzika mapema. Alijitoma chumbani na kuanza kukoroma mara moja. Panya alitabasamu, akatikisa kichwa na kuelekea ghalani kuendeleza shughuli zake.

Binadamu alimfuata nyuma kwa kunyatanyata. Mle ghalani, kulitokea sauti kama ya mashine inayosaga mahindi. Kitufe fulani kilimkaba Binadamu kooni akakifungua kilango na kujitoma ghalani. Wawili hawa walitazamana, kila mmoja amepigwa na butwaa. Hapakuwa na jingine. Urafiki wa viumbe hawa uliishia hapo.

5. Kulingana na **aya ya kwanza,** Panya alimsaidia Binadamu kwa

______________________________________________

6. Ni kauli gani ambayo **haionyeshi** kuwa hadithi hii inahimiza uhusiano mwema?
   A. Panya kumjuza Binadamu kuhusu hatari iliyomkabili.
   B. Panya kufikiri kwa muda kabla ya kumhukumu Binadamu.
   C. Binadamu kumhakikishia Panya haki za kimsingi.
   D. Binadamu kuamua kwamba magunia yaliharibiwa na ukuukuu.

7. 'Urafiki wa viumbe hawa uliishia hapo.' Unadhani kulitokea nini baada ya urafiki huo kuisha?

______________________________________________

______________________________________________

8. Kauli, **“Kwa nini nile ukoko na chungu kimejaa chakula ndi?”** inamaanisha kuwa Panya:
   A. analalamika
   B. anajuta
   C. anahofu
   D. anashuku

**UFUPISHO**

*Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la* ***9*** *hadi* ***12****.*

Mto ni nini? Mto ni njia yenye maji yanayotiririka na kufanya mkondo hasa kuanzia milimani hadi baharini. **Mito hutofautiana kwa kina, urefu na upana. Nchini Kenya kwa mfano, Mto Tana ndio mrefu zaidi. Aidha, kasi ya kutiririka kwa maji kwenye mto hutegemea nguvu za msukumo wa maji kutoka maeneo ya juu kuelekea chini.**

Umuhimu wa mito hauwezi kupuuzwa. Mito hufanikisha shughuli za kilimo. Mathalani, maji ya mito hutumiwa kunyunyizia mashamba ili kupata mavuno ya kutosha. Isitoshe, watu hutumia mito kwa usafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine. Kupitia vyombo vya usafiri kama vile madau, bidhaa husafirishwa hadi kwenye masoko yaliyo upande mwingine wa mto. Kwa njia hii, mito hurahisisha ubadilishanaji wa bidhaa na huduma, hivyo kuendeleza shughuli za ukuzaji wa uchumi.

Ikumbukwe kwamba, mito ni hifadhi ya viumbe wa majini kama vile samaki ambao humfaa binadamu. Kadhalika, maji ya mito humfaa binadamu kwa matumizi ya nyumbani kama vile kunywa, kupikia na kufanyia usafi. Ni jukumu la kila mwanajamii kuitunza mito ili kunufaika vilivyo kutoka kwayo.

9. Eleza maana ya mto kwa maneno yasiyozidi **sita.**

_______________________________________________

_______________________________________________

10. Andika ujumbe wa kauli zilizokolezwa rangi katika **aya ya kwanza** kwa maneno yasiyozidi **15.**

_______________________________________________

11. Kwa maneno **15**, eleza manufaa ya mito katika ukuzaji wa uchumi.

_______________________________________________

12. Fupisha ushauri anaotoa mwandishi katika **aya ya mwisho** kwa maneno **6.**

_______________________________________________

**Geuza ukurasa**

**ZOEZI 4: SARUFI**

Ni wazi kuwa mitandao _13___manufaa mengi ulimwenguni . _14_ , ni vyema kujihadhari ili _15___ uhalifu wa mitandaoni. Tuhakikishe kuwa __16__ tovuti salama kila mara. Aidha, tuwachunguze wanaodai kuwa marafiki wetu mitandaoni kwani _17__ .

13. A. yameleta B. imeleta C. zimeleta D. umeleta

14. A. Kwa sababu B. Angalau C. Ilhali D. Hata hivyo

15. A. kuzuia B. kuzuilia C. kuzuiwa D. kuzuiliwa

16. A. tukifungua B. tunafungua C. tutafungua D. tungefungua

17. A. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.
    B. Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi.
    C. Usilolijua ni usiku wa giza.
    D. Mwenye pupa hadiriki kula tamu.

18. Neno 'mradi' katika sentensi: Tumeanzisha mradi wa kufuga kuku, ni nomino. Onyesha kivumishi na kielezi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

    Mama atauza matunda mabivu kesho.

    ______________________________________________

    ______________________________________________

19. Geuza sentensi ifuatayo iwe katika wakati uliopita hali timilifu (alama 2)

    Koja atapalilia shamba kwa jembe hili.

    ______________________________________________

20. Neno 'Huyo' katika sentensi, Huyo ni mwigizaji hodari ni kiwakilishi kiashiria. Tunga sentensi moja ukitumia kiwakilishi kimilikishi.
    (alama 2)

    ______________________________________________

21. Jaza nafasi katika jedwali. Fuata mfano. (alama 2)

| upesi | polepole |
|---|---|
| Jenga | |
| Kaza | |

22. Andika ukanusho wa sentensi ifuatayo: Juma alibuni kisa cha kusisimua. (alama 1)

23. Tunga sentensi ukitumia neno ‘kibanda’ katika hali ya ukubwa. (alama 2)

24. Andika wingi wa:

Tumia ujana wako kwa faida ya jamii yako. (alama 2)

25. Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 2)

“Nisomee aya hii ili nitathmini jinsi unavyotamka.” Tamara alimwambia mwenzake.

**Geuza ukurasa**

**ZOEZI 5: KUANDIKA (alama 10)**

26. Mzazi au mlezi wako amekununulia kipakatalishi cha kukusaidia katika ujifunzaji. Mwandikie barua kumshukuru.

**SEHEMU YA C: FASIHI**

**ZOEZI 6: FASIHI SIMULIZI** **(alama 10)**

27. *Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Hapo zamani za kale nyani waliishi katika msitu mmoja mpana kama bahari. Mmoja wa nyani hao alikuwa na akili iliyokamata kama sumaku. Hakuna mtego hata mmoja uliomshika; alibuni mikakati na **kuibwaga chini pu!** Wenzake hawakuacha kuajabia wepesi wa akili yake.

Siku moja, nyani walishambuliwa na fisi. **Waliingiwa na hofu wakatetemeka hivi,** utadhani ni jani wakati wa upepo mkali. Hakuna aliyemwazia mwenzake; ilikuwa mguu niponye. Wote walitifua kivumbi kuelekea upande wa mashariki isipokuwa nyani wetu mwenye akili nyepesi. Huyu alijitoma kwenye shimo lililokuwa karibu, akajibanza kwenye upenyu mmoja wa shimo hilo na kujikaukia kama ukuni.

Fisi waliojawa na furaha kwa kupata kitoweo walilipita shimo hilo hapo hapo wakifuata wale nyani wengine. Walikimbia huku mate yakiwadondoka ndo ndo ndo! Ungewaona ungecheka hadi mbavu zivunjike. Fisi walizidi kukimbia. Walikimbia, wakakimbia, wakakimbia-a-a.... Hata walipofika ukingoni mwa mto mmoja mkubwa waligundua kwamba juhudi zao zilikuwa za mfamaji. Kitoweo chao kilikuwa kimewadondoka viganjani. Walibaki kutiririkwa na machozi tiriri.

Huko nyuma, yule nyani wetu alibaki kuwahurumia wenzake kwa yale ambayo yangewafika. "Laiti wangalikuwa kama mimi!" Alijisemea huku akitoka kwenye shimo. Hadithi yangu inaishia hapo.

a) Hii ni hurafa. Thibitisha kwa kutoa mifano miwili. (alama 2)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

b) Eleza ujumbe wa hadithi hii. (alama 2)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

c) Kauli, **kuibwaga chini pu!** imetumia tanakali za sauti. Bainisha vipengele vingine vya lugha vilivyotumiwa kufanikisha uwasilishaji wa hadithi hii. (alama 2)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

d) Fikiria kwamba wewe ndiye fanani wa hadithi hii. Utawasilisha vipi kauli ifuatayo? **Waliingiwa na hofu wakatetemeka hivi,** (alama 2)

______________________________________________________________

Geuza ukurasa

e) Eleza sifa **mbili** za nyani aliyejificha shimoni kwa kurejelea **aya ya mwisho**.

(alama 2)

_______________________________________________________________

28. **ZOEZI LA 7: TAMTHILIA** **(alama 10)**

*Soma sehemu ifuatayo ya tamthilia kisha ujibu maswali.*

**SEHEMU YA PILI**

**ONYESHO LA KWANZA**

*(Ni asubuhi, mwendo wa saa mbili. Shaibu mmoja, Okilo, ameketi chini ya mbuyu ulio mkabala na nyumba moja ya msonge. Kando yake kuna mikongojo miwili. Anaikazia macho huku amezama katika fikira. Mara Chifu anafika.)*

**Okilo:** (*Akijaribu kuinuka ili kumkaribisha.*) Bwana Chifu, karibu huku kwetu.

**Chifu**: (*Akimnyoooshea mkono.*) Sabalkheri Ndugu Okilo!

**Okilo**: (*Akimpa mkono.*) Akheri, Bwana Chifu. U mzima? Natumai hamna aliyevunja sheria huku kwangu! (*Anacheka.*)

**Chifu**: (*Akicheka vilevile.*) Ni mzima Ndugu Okilo, nashukuru Mungu. Usiwe na shaka. Huku kwenu mmetakata mkawa weupe kama pamba. Naona unafurahia miale ya jua changa. Mkeo hajambo?

**Okilo:** (*Akiitikia kwa kutikisa kichwa.*) Hajambo. Msimu huu wa matayarisho ya upanzi yeye huwa na hekaheka nyingi. Akitoka macheo anarudi mafungia ng'ombe.

**Chifu:** (*Akionyesha makini zaidi.*) Ehee! Inabidi. Wajua ajizi ni nyumba ya njaa.

**Okilo:** (*Akitikisa kichwa kukubali*) Kweli kabisa Bwana Chifu. Laiti ningalikuwa na uwezo wa kusaidia kule shambani!(*Kimya kidogo*.) Mimi humsaidia tu kwa shughuli nyepesi kama vile kukoboa mahindi na kumtazamia hao mbuzi wetu aliowafunga.

**Chifu***:* (*Akionyesha masikitiko.*) Hata hiyo ni kazi mwenzangu. Usijilaumu. Kuna wengi waliojaliwa uzima wa miili lakini hawashiriki katika ujenzi wa taifa. Angalau wewe huyafanya hayo madogo. Hata hivyo, si neno. Mungu humpa alalaye na aamkaye.

**Okilo***:* (*Akichangamka.*) Kweli Bwana Chifu. Nashukuru kwa uwezo mdogo nilio nao.

**Chifu:** Papo hapo ndipo palipo na kiini cha kufika hapa siku ya leo. (*Akisafisha koo.*) Serikali inatambua changamoto wanazopitia watu wenye mahitaji maalumu kama wewe. Inaendesha shughuli ya kuwasajili watu hao ili kubaini mahitaji yao. (*Akitoa faili kwenye mkoba.)*

**Okilo:** (*Macho yaking'aa kwa furaha.)* Ahaa! Hiyo ni hatua muhimu kwetu. Asante sana Bwana Chifu kwa kunifikiria. Ila sioni kama kuna mengi ya kukueleza. Hali yangu unaiona na kuifahamu fika.

**Chifu:** *(Akichukua kalamu.)* Usiwe na wasiwasi kakangu. Ni jukumu letu. *(Kimya kidogo.)* Nayaelewa mahitaji yako ya kimsingi. Wewe unahitaji kitimaguru kukurahisishia kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine.

**Okilo:** Naam, Bwana Chifu umegonga ndipo. Ikiwezekana, ongezea miwani hapo. Siku hizi naona vimulimuli tu; pengine ni huu umri unaonichongea. (*Anachekacheka.*)

**Chifu:** (*Akicheka.*) Sawa kakangu. Nitafanya mpango utembelewe na mtaalamu wa macho. Kisha, vifaa hivi vitakapofika nitakukabidhi mimi mwenyewe.

**Okilo:** Nitashukuru sana Bwana Chifu.

**Chifu:** (*Akisimama.*) Karibu. Ninaomba niondoke ili niwahi kwingine.

(*Wanaagana.*)

(*Taa zinazimika*.)

a) Maudhui ni masuala ambayo yanazungumziwa katika kazi ya fasihi. Eleza masuala **mawili** yanayojitokeza katika sehemu hii ya tamthilia. (alama 2)

____________________________________________________________

b) Eleza umuhimu wa mandhari kwa kurejelea sehemu hii ya tamthilia.

(alama 2)

____________________________________________________________

____________________________________________________________

c) Fafanua sifa **tatu** za Okilo kwa mujibu wa onyesho hili. (alama 3)

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

d) Katika onyesho hili, **umri unaonichongea** ni tashihisi. Eleza vipengele vingine **vitatu** vya lugha vilivyotumiwa katika onyesho hili. (alama 3)

____________________________________________________________

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**